JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA KILIMO

TPHPA

TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

# MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA



# UDHIBITI HUSISHI WA VISUMBUFU VYA VIAZI MVIRINGO

## Minyoo fundo
## (Root Knot Nematodes)

**Utangulizi**

Ugonjwa huu hushambulia mizizi yna kuharibu viazi mviringo kwa kusababisha vifundofundo .

**Dalili za mashambulizi**



- Kunyauka kwa mmea,
- Majani hubadilika rangi na kuwa ya njano

## Dalili za ugonjwa




- Kunyauka kwa mmea majani yakiwa bado na rangi ya kijani,
- Kiazi hutoa utomvu mweupe wa bakteri

## Mnyauko bakteri
## (Bacterial wilt)

**Utangulizi**

Mnyauko bakteria ni ugonjwa unaosababishwa na bakteria wanaoishi kwenye udongo na vyanzo vya maji, ambao hushambulia mmea kupitia kwenye mizizi na kuzaliana kwa wingi kisha huziba njia ya mmea kupitisha maji.

## Mnyauko fusari
## (Fusarium wilt)



Majani hua ya njano kwanza, kisha hunayuka na hubadilika kua na rangi ya kahawia

## Bakajani chelewa (Late blight)

### Utangulizi

Ugonjwa huu unaweza kutokea wakati wowote kuanzia kitaluni hadi shambani. Ugonjwa huu hutokea baada ya mvua nyepesinyepesi ya muda mrefu kunyesha.

### Dalili za ugonjwa







Majani, matunda na shina hupata mabaka ya rangi ya kahawia hadi nyeusi. Mabaka yake yana majimaji na wakati mwingine hupata kuvu inayonekana kama utandu mweupe.

## Bakajani tangulia (Early blight)

### Utangulizi

Ugonjwa husababishwa na vimelea vya ukungu ambavyo hutokea wakati wowote kwenye msimu.

### Dalili za ugonjwa



Kuonekana kwa kuvu nyeusi yenye viduara vingi vya mviringo kwenye majani ya chini na matunda . Kovu kwenye jani huzungukwa na rangi ya njano pembeni

### UDHIBITI HUSISHI WA MAGONJWA

1 Tumia mbegu bora zilizothabitishwa.

2 Tumia mbegu za viazi mviringo zenye sifa kinzani kwa magonjwa.

3 Panda miche kwa masafa yaliyokubalika kitaalamu kuwezesha mzunguko wa hewa shambani.

4 Palilia shamba na eneo linalozunguka shamba kudhibiti magugu.

5 Ng'oa na angamiza masalia kwa kuchoma moto.

6 Tumia mbolea za samadi, mboji na hata za viwandani kuboresha afya ya mimea, zitumike kwa kufuata ushauri wa wataalam wa kilimo.

7 Tumia viuatilifu pale inapofaa kwa viwango sahihiikibidi tafuta ushauri wa wataalam wa kilimo.

8 Lima kilimo cha mzunguko kwa kutumia mazao yasio ya jamii moja na viazi mviringo (mfano kabichi, bamia, matango, tikitimaji n.k).

## Muozo laini



### Utangulizi na Dalili

Ugonjwa huu husababishwa na backateria. Kiazi hulainika na kujaa majimaji. Utomvu honekana kwenye macho. Kiazi hua kama kama kimeiva.









### Mnyauko fusari (Fusarium wilt)



Majani hua ya njano kwanza, kisha hunayuka na hubadilika kua na rangi ya kahawia

### Bakajani tangulia (Early blight)



### Bakajani chelewa (Late blight)





**PIGA SIMU BURE:**

**080 011 003 1**

P.O. Box 3024 , Arusha - Tanzania Nairobi Rd, Ngaramtoni Area

| Phone | Web | Email |
|---|---|---|
| +255 739 970 467 | www.tphpa.go.tz | dg@tphpa.go.tz |

tphpa_tz   tphpa_tz   TPHPA HABARI TV

SCAN FOR MORE